

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

03 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 03 MEI, 2021

I. DUA:

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa

majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**168. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO
KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Utaratibu wa Watoto kuingia darasa la Kwanza ni lazima awe amepitia Shule za awali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha madarasa ya Elimu ya Awali.

**169. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO
RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa maboma ya Vituo vya Afya yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi katika Kata za Makuro na Ngimu.

WIZARA YA MAJI:

170. MHESHIMIWA ALEXANDER PASTORY MNYETI (MISUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji kwenye Mji wa Usagara.

171. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANGH'WALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- Je, ni lini mradi wa Maji wa kutoka Nyamtukuza, Kakora, Kharumwa, Izunya, Kayenze hadi Bukwimba utakamilika.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

172. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanja cha Ndege cha Mwada Mkoani Manyara.

**173. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA
(KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Daraja la
Mto Butu ili Wananchi wa upande wa pili wa
Mto waweze kuvuka na kupata huduma
mbalimbali za kijamii.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**174. MHESHIMIWA MOHAMED SULEIMAN
OMAR (MALINDI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya
Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Askari
wavya pamoja na kuleta vitendea kazi vya
kutosha kwa Polisi Zanzibar inayokabiliwa na
upungufu mkubwa wa Askari kutokana na
wengi kufikia umri wa kustaafu.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO:**

**175. MHESHIMIWA RAVIA IDARUS FAINA
(MAKUNDUCHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,
Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kwa nini Vyama vya michezo ikiwemo TFF na TOC vimekuwa vikibadili Katiba zao kwa lengo la kulinda Viongozi waliopo madarakani na kudhibiti Watanzania wengine wasigombe nafasi katika Vyama hivyo.

WIZARA YA MADINI:

176. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inafahamu madhara yatokanayo na Madini ya Zebaki.

WIZARA YA KILIMO:

177. MHESHIMIWA DKT. PINDI HAZARA CHANA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutafuta Soko la uhakika la zao la Mahindi kwa Wakulima wa Mikoa ya Kusini hususan Mkoa wa Njombe.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**178. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Tarafa ya Mahenge Wilayani Kilolo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
03 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**